ISSN 2820-2686 | Toleo Na. 6 | Januari - Machi 2023

# JARIDA LA WAKILI MKUU







osgtanzania osg_tanzania WAKILI MKUU TV Email: info@osg.go.tz www.osg.go.tz

# BODI YA UHARIRI

## Mwenyekiti

Sarah Duncan Mwaipopo
Naibu Wakili Mkuu wa Serikali

## Mhariri Mkuu

Prisca Jackson Ulomi
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

## Waandishi wa Jarida

Prisca Jackson Ulomi
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

Sarah Obby Mwakyusa
Afisa Habari Mwandamizi

Dennis Julius Buyekwa
Afisa Habari

## Msanifu wa Jarida

Nyamhoni Robert Chacha
Afisa TEHAMA

## Wajumbe

George Nathaniel Mandepo
Mkurugenzi wa usuluhishi

Hangi Matekeleza Chang'a
Mkurugenzi Msaidizi Katiba, Haki za Binadamu na Uchaguzi

Kiuye Mbwana Shemakame
Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Maktaba na Utafiti

CPA Devota Mathew Ngulugulu
Mhasibu Mkuu

Mercy Rowland Kyamba
Mkurugenzi Msaidizi - Udhibiti Ubora

Zuhura Mohamed Kussaga
Mchumi

# TAHARIRI

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ina jukumu la kuratibu, kusimamia na kuendesha mashauri yote ya madai, usuluhishi, Katiba na Haki za Binadamu kwa niaba ya Serikali na taasisi zake nchini. Ofisi hii ilianzishwa kwa lengo kuimarisha Sekta ya Sheria nchini hasa katika usimamizi wa mashauri ya madai na usuluhishi.

Ofisi hii imehakikisha inaendelea kujitangaza kwa wadau wake ili waweze kuyafahamu majukumu ya Ofisi kwa kwakufanikisha dhumuni hili, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeendelea kushiriki kikamilifu kwenye Maadhimishio ya Wiki ya Sheria nchini ambapo maaadhimisho haya huadhimishwa kila mwaka kwa kuratibiwa na Mahakama ya Tanzania ikiwa ni kuashiria kuanza kwa mwaka mpya wa Mahakama nchini.

Maadhimisho ya Wiki ya Sheria nchini yana umuhimu mkubwa katika kuelimisha na kuhamasisha jamii kuhusu sheria, haki na wajibu. Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kama mdau muhimu kwenye Sekta ya Sheria iliweza kushiriki kikamilifu katika Wiki ya Sheria ambapo pamoja na mambo mengine ilihusika katika kuwawezesha wananchi na wadau kwa ujumla kufahamu majukumu ya Ofisi kwa ufasaha.

Hatua hiyo ililenga katika kuwawezesha wadau wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kutambua kikamilifu namna ambavyo Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inavyotekeleza majukumu yake kwa kuzingatia sheria, taratibu na kanuni na madhumuni ya kuundwa kwa Ofisi hii.

Hivyo, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeendelea kuonesha dhamira yake ya dhati katika kushirikiana na wadau wengine ili kuhakikisha kuwa wote kwa pamoja tunaendelea kujenga jamii inayozingatia misingi ya haki, usawa, utii wa sheria, utawala bora na kufanikisha upatikanaji wa haki kwa wakati kutoka kwa watekelezaji wa mnyororo wa haki nchini.

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeendelea kuwashirikisha watumishi wake kwenye mipango ya Ofisi kupitia vikao vya Baraza la Wafanyakazi. Vikao vya Baraza hilo ni utekelezaji wa takwa la kisheria la kuwashirikisha wafanyakazi katika uongozi wa pamoja mahala pa kazi kwa mujibu wa Kanuni Na. 108 ya Kanuni za Utumishi wa Umma za Mwaka 2003 pamoja na Kifungu cha 73 cha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya Mwaka 2004 na Kifungu cha 30 (3) cha Sheria ya Majadiliano ya Pamoja na Kanuni Na. 24 ya Kanuni za Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Umma za Mwaka 2005.

Vikao vya Baraza la Wafanyakazi ni muhimu katika kuongeza ufanisi na tija kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kuwa kupitia vikao hivi wafanyakazi wanapata fursa ya kutoa maoni yao ya kuboresha utendaji kazi. Ushirikishwaji wa wafanyakazi unawaleta watumishi pamoja katika kutekeleza Sera za Serikali, kujenga motisha, kuinua ari na morali kwa watumishi wa umma kwa maendeleo ya taasisi na taifa kwa ujumla.

Ni matumaini yetu kuwa wadau na wananchi wataendelea kuipa ushirikiano Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ili kuwa na mikakati na mipango endelevu ya pamoja kwa lengo la kufikia azma ya kuwa chachu ya maendeleo na maslahi mapana ya Ofisi na Taifa kwa ujumla.



**Prisca Jackson Ulomi**
**Mhariri Mkuu**



# Kutoka Kwenye Dawati la Mwenyekiti wa Bodi ya Uhariri



**Sarah D. Mwaipopo**

**Naibu Wakili Mkuu wa Serikali**



Toleo la Sita la Jarida la Wakili Mkuu wa Serikali ni maalumu kwa ajili ya kuendelea kuangazia mafanikio ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika miaka miwili ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ofisi kupitia Jarida hili inatambua mchango mkubwa wa Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan katika maeneo ya bajeti, ujenzi wa Ofisi ya makao makuu jijini Dodoma, usimamizi wa mashauri, udhibiti ubora, mafunzo kwa watumishi, ushirikiano wa Ofisi na wadau, maboresho ya mifumo ya TEHAMA na ununuzi na makabidhiano ya magari ya Ofisi za mikoa ambayo kwa kiasi kikubwa yameboresha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hii.

Pamoja na mafanikio haya yanayotokana na mchango mkubwa wa Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imekuwa mstari wa mbele katika kuhimiza na kusisitiza masuala mtambuka ikiwemo masuala ya kijinsia, nafasi ya watumishi katika kukuza uadilifu na utunzaji wa siri za Serikali.

Pia, Toleo hili linaangazia ushiriki wa OWMS katika Maadhimisho ya Kilele cha Wiki ya Sheria na Baraza la Wafanyakazi pamoja na nafasi ya Ofisi katika kutatua migogoro kwa njia ya usuluhishi. Vile vile, linaangazia nafasi ya Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS) katika kuwajengea uwezo wanachama wake. Hii ni kutokana na kwamba TLS ni mdau muhimu wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kuwa hiki ni chama cha kitaaluma kwa wanasheria.

Aidha, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ni mdau mkubwa katika kukuza uchumi wa Taifa katika utekelezaji wa majukumu yake ya kuiwakilisha Serikali na taasisi zake katika Mahakama na mabaraza. Katika jambo hili, Toleo hili linaangazia nafasi ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika kuokoa fedha za Serikali kupitia mashauri. Matukio yote haya ni sehemu ya utendaji kazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na wadau wake hususan Serikali na taasisi zake chini ya uongozi wa Rais Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan.

Naomba nimalizie kwa kuwaomba wasomaji wetu kuendelea kutoa maoni kwa Bodi ya Uhariri kwa ajili ya maboresho ya Jarida hili ili kwa pamoja tuweze kulifanya jarida hili kutoa mchango chanya katika ukuaji wa Sekta ya Sheria nchini pamoja na kuboresha utendaji na ufanisi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali. Nawatakia usomaji mwema wa Toleo la Sita la Jarida la Wakili Mkuu. Asanteni.

# Yaliyomo


06 Mafanikio ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Katika Kipindi cha Miaka Miwili ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan

11 Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Yashiriki Kilele cha Maadhimisho ya Wiki ya Sheria

16 Wadau Watakiwa Kutatua Migogoro kwa Njia ya Usuluhishi

22 Naibu Waziri Gekul Aipongeza Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali

28 TLS Yatakiwa Kuwajengea Uwezo Wanachama Wake

31 Serikali Yasisitiza Uzingatiaji wa Usawa wa Kijinsia, Ubunifu na Mabadiliko ya Teknolojia

36 Zingatieni Uadilifu na Usiri wa Nyaraka za Serikali




# Mafanikio ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Katika Kipindi cha Miaka Miwili ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan






## UTANGULIZI

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (OWMS) ilianzishwa kupitia Amri ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliyotangazwa tarehe 13 Februari, 2018 (Tangazo la Serikali Na. 50 la Mwaka 2018). Amri hiyo ilitolewa na Mhe. Rais kwa mujibu wa Ibara ya 36 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977.

Kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na. 50 la Mwaka 2018, uanzishwaji wa OWMS ulilenga kuiwezesha Serikali kusimamia, kuendesha na kuratibu mashauri ya madai na usuluhishi ndani na nje ya nchi. Hii inajumuisha kuiwakilisha Serikali katika Mahakama zote za ndani na nje ya nchi na Mabaraza ya Usuluhihisi wa Migogoro ya Kitaifa na Kimataifa.

Lengo kuu la kuanzishwa kwa OWMS ni kuwa na taasisi moja ya kiserikali inayowajibika na uratibu, usimamizi na uendeshaji wa mashauri yote ya madai na usuluhishi yanayofunguliwa na Serikali/ taasisi zake au dhidi ya Serikali/taasisi zake ndani na nje ya nchi. Malengo mengine ni pamoja na kujenga taasisi yenye uwezo wa kitaalamu ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

> Katika kipindi cha miaka miwili (Machi 2021 hadi Machi, 2023) ya uongozi wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mafanikio makubwa yamepatikana.

# Mafanikio

## 01 Bajeti

Katika kipindi cha miaka miwili ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali iliongezewa bajeti kutoka shilingi bilioni 11.48 kwa Mwaka wa Fedha 2020/21 hadi bilioni 12.13 kwa Mwaka wa Fedha 2021/22 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 5.4 na Mwaka wa Fedha 2022/23 ilipatiwa shilingi bilioni12.81.

Kuongezeka kwa bajeti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kumefanikisha utekelezaji wa majukumu ya uendeshaji wa shughuli za Ofisi hasusan katika uendeshaji mashauri ya madai na usuluhishi kwa niaba ya Serikali na taasisi zake na kupunguza changamoto za ufinyu wa bajeti zilizokuwepo awali.

## 02 Usimamizi wa mashauri ya madai na usuluhishi

Katika kipindi cha miaka miwili ya Serikali ya Awamu ya Sita, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imefanikiwa kuiwakilisha Serikali kwa kuendesha jumla ya mashauri 5,993 yakiwemo mashauri 5,854 ya madai na mashauri 139 ya usuluhishi. Hivyo, kuweza kuepuka gharama kubwa za kutumia Mawakili wa kujitegemea na kuokoa fedha ambazo zingelipwa endapo Serikali ingeshindwa. Aidha, Ofisi imeweza kusimamia na kushinda mashauri ya madai na usuluhishi yanayohusisha mali na fedha kama vile mashauri ya ardhi na uwekezaji katika sekta mbalimbali; na mashauri yasiyohusisha mali na fedha kama vile mashauri ya katiba, haki za binadamu na uchaguzi.

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeongoza na kushiriki katika Timu za Serikali za Majadiliano (GNT) na kufanikisha kumaliza mashauri/migogoro mbalimbali kwa njia ya majadiliano, usuluhishi na maridhiano nje ya Mahakama; Kupitia majadiliano hayo, Ofisi imeweza kuokoa fedha, kumaliza migogoro kwa muda mfupi, kujenga imani kwa wawekezaji na kurudisha mahusiano kwa wadau kwenye sekta mbalimbali za uchumi na jamii.

## 03 Kuimarisha Mifumo ya Usimamizi wa mashauri na Udhibiti wa Ubora

Katika kipindi cha miaka miwili ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita, OWMS imeimarisha Mfumo wa Usimamizi wa Mashauri (Case Inventory Management System), kufanya ufuatiliaji wa mienendo ya mashauri na kupitia sheria zinazohusu mashauri ya madai na usuluhishi. Pia, Ofisi imeweza kuandaa miongozo ya kusimamia na kudhibiti viwango vya ubora vya Mawakili wa Serikali katika uendeshaji wa mashauri.Vile vile, Ofisi imeweza kuandaa Mkataba wa Huduma kwa Mteja kwa ajili ya Serikali na taasisi zake.

## 04 Mafunzo kwa Watumishi

Kupitia Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Serikali ya Awamu ya Sita imewezesha watumishi 647 kupata mafunzo, kati yao watumishi 30 wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu, 117 mafunzo ya muda mfupi na Mawakili 500 kutoka Wizara, TAMISEMI na taasisi mbalimbali za Serikali ikiwemo; NSSF, TPA, NHC, NIDA, EPZA, UDSM, OUT, TIB TCRA, TPDC na PSSSF walipatiwa mafunzo maalum ya uendeshaji wa mashauri.

## 05 Ujenzi wa Ofisi

Ofisi ya Wakili wa Serikali inaendelea na ujenzi wa jengo la makao makuu ya Ofisi katika Mji wa Serikali Mtumba, Dodoma lenye ukubwa wa mita za mraba 17,342 unaotarajiwa kugharimu kiasi cha shilingi 26,740,706,111.79 ambacho kinajumuisha gharama za mkandarasi kiasi cha shilingi 26,242,926,061.79 na mshauri elekezi kiasi cha shilingi 497,780,050.00. Kipindi cha mradi ni miezi 18 kuanzia mwezi Julai, 2022.

## 06 Ununuzi wa Magari ya Ofisi

Ili kuwezesha kuleta ufanisi katika kutekeleza majukumu nyeti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ambayo yanahusisha uendeshaji wa mashauri Mahakamani na kwenye Mabaraza ya Usuluhishi, Serikali imeiwezesha OWMS kununua magari mapya 16 na kufanya Ofisi kuwa na jumla ya magari 31. Kuongezeka kwa idadi ya magari kumesaidia kuwa na usafiri wa uhakika ambao unarahisisha utekelezaji wa majukumu hayo na kuleta ufanisi katika utekelezaji.

## 07 Kuboresha Ushiriki wa Wadau na Uimarishwaji wa Taratibu pamoja na Miundombinu ya TEHAMA

Katika kipindi cha miaka miwili ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Ofisi imeendelea kuanzisha na kuboresha mifumo mbalimbali ya TEHAMA. Katika kipindi hicho Ofisi imeweza kubuni na kuanzisha mfumo wa kuhifadhi nyaraka za maktaba (OSG e-library) wenye lengo la kuwezesha upatikanaji wa nyaraka za rejea kwa ajili ya uendeshaji wa mashauri na tafiti. Aidha, Ofisi imeendelea kuboresha mfumo wa usimamizi wa taarifa za mashauri (CIMS).

Katika kipindi hiki, Ofisi imeweza kununua kompyuta mpakato (laptop) 68 za nyongeza na kompyuta za mezani 35 (desktop), seti mbili za vifaa vya kufanyia majadiliano na kuendesha mashauri kimtandao (Video Conference), seva kwa ajili ya kuhifadhia taarifa mbalimbali za Ofisi na vifaa mbalimbali kwa ajili ya uendeshaji wa Ofisi.


Pia, Ofisi imeendelea kuelimisha/kuhabarisha umma kwa kutoa taarifa mbalimbali za OWMS kwa wadau na wananchi kwa ujumla ikiwemo uchapishaji wa nakala 2,250 za Jarida la Wakili Mkuu; makala 120; machapisho na vipeperushi 750; vipindi maalum vitatu vya runinga; mabango ya mtandaoni 25; kuchambua na kuweka taarifa za Ofisi kwenye tovuti ya Ofisi (www.osg.go.tz:) na mitandao ya kijamii.

## 08 Kufungua Ofisi za Mikoa

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeendelea kujiimarisha kwa kufungua Ofisi za Mikoa ili kupeleka huduma karibu na taasisi na Ofisi za Serikali zilizopo katika mikoa husika pamoja na wananchi. Katika kipindi cha miaka miwili Ofisi mbili zimefunguliwa katika mikoa ya Morogoro na Rukwa na kufanya OWMS kuwepo kwenye mikoa 17 yenye Masijala za Mahakama Kuu. Aidha Ofisi ina mpango wa kuendelea kufungua Ofisi kwa kila mkoa ulio na Masijala ya Mahakama Kuu nchini.

## HITIMISHO

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali itaendelea kuunga mkono jitihada za Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa kutekeleza jukumu la kuratibu, kusimamia na kuendesha mashauri kwa ufanisi na weledi kwa niaba ya Serikali na taasisi zake ili kuhakikisha pato la Taifa na uchumi wa nchi unaongezeka kwa kutetea na kulinda maslahi ya Serikali ipasavyo ndani na nje ya nchi.



# Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Yashiriki Kilele cha Maadhimisho ya Wiki ya Sheria

**Utatuzi wa Migogoro kwa njia ya usuluhishi katika Kukuza Uchumi Endelevu**




## MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN
**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan akihutubia viongozi mbalimbali pamoja na Majaji walioshiriki Maadhimisho ya Kilele cha Wiki ya Sheria Tanzania yaliyofanyika tarehe 1 Februari, 2023 katika viwanja vya Chinangali Jijini Dodoma.*

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali tarehe mosi Februari, 2023 imeshiriki kilele cha Maadhimisho ya Wiki ya Sheria nchini ambapo Mgeni Rasmi alikuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan huku Ofisi ikiwakilishwa na Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Bi. Sarah Duncan Mwaipopo pamoja

na baadhi ya Mawakili wa Serikali.

Akizungumza katika maadhimisho hayo yaliyofanyika kitaifa katika Viwanja vya Chinangali jijini Dodoma yenye kauli mbiu isemayo, "Umuhimu wa Utatuzi wa Migogoro kwa Njia ya Usuluhishi katika Kukuza Uchumi Endelevu: Wajibu wa Mahakama na Wadau", Mhe. Rais Dkt. Samia amefurahishwa na juhudi zinazofanywa na Mahakama ya Tanzania pamoja na wadau wake kwa kazi nzuri ya kuhakikisha wanatoa haki kwa usawa na kwa wakati.

Mhe. Rais Dkt. Samia ameongeza kuwa mafanikio makubwa yaliyofikiwa yamechangiwa na uamuzi wa Serikali uliofanywa mwezi Agosti, 2022 wa kuongeza idadi ya Majaji wa Mahakama Kuu kutoka Majaji 78 waliokuwepo hapo awali mpaka kufikia Majaji 100 hatua ambayo imeongeza chachu katika kufikia mafanikio hayo.

Mhe. Rais Dkt. Samia ameeleza kuwa kwa sasa Majaji wote nchini wanaendelea kutoa haki kwa usawa na kwa wakati kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za utoaji haki nchini pasipo kumuonea mtu yoyote.

Pia, Mhe. Rais Dkt. Samia ameipongeza Mahakama kwa ujenzi wa miundombinu na kuendelea kusogeza huduma karibu na wananchi huku akionyesha kufurahishwa zaidi na hatua zilizofikiwa za kukamilika kwa taratibu za upatikanaji wa huduma za Mahakama Kuu katika mikoa minane ya Singida, Pwani, Songwe, Katavi, Geita, Njombe, Simiyu na Lindi sambamba na mpango wa kujenga vituo jumuishi vya utoaji haki katika maeneo mengine ikiwemo kisiwani Pemba.

Kuhusu suala la upungufu wa watumishi pamoja na maslahi kwa watumishi wa Mahakama, Mhe. Rais Dkt. Samia ameahidi kuendelea kulifanyia kazi suala hilo kwa kuanza na hatua ya kuunda Kamati ambayo italifanyia kazi na kutoa taarifa yake baada ya miezi minne.

Mhe. Rais Dkt. Samia ameeleza kutambua uwepo wa fedha kutoka kwa wadau wa maendeleo ikiwemo Benki ya Dunia ambazo zimesaidia kuimarisha miundombinu ya Mahakama, ikiwemo Mahakama za Mwanzo 60 na majengo mengine 18 ambapo kati ya hayo Mahakama za Wilaya ni kumi na moja.

"Uwepo wa majengo haya ni ishara nyingine na azma ya Mahakama pamoja na Serikali kuhakikisha inasogeza huduma za haki karibu na wananchi hivyo naomba kutoa rai kwa uongozi wa Mahakama kuwa miradi yote inayotekelezwa izingatie ubora unaoendana na fedha iliyotolewa," alisema Mhe. Rais Dkt. Samia.




*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Bi. Sarah Mwaipopo (aliyesisima mbele kushoto) akiwa tayari kushiriki kilele cha Maadhimisho ya wiki ya Sheria yaliyofanyika katika Viwanja vya Chinangali Jijini Dodoma. Kulia ni Mhe. Sharmillah Sarwatt, Msajili wa Mahakama Kuu ya Tanzania.*

Mhe. Rais Dkt. Samia amesisitiza kuwa azma ya Serikali yake ni kuhakikisha taasisi zinazoshirikiana na Mahakama katika mnyororo wa utoaji haki, ikiwemo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka pamoja na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali zinapata pia miundombinu wezeshi ili shauri litakalofunguliwa Mahakamani lisomeke sawa sawa na lile lililosajiliwa katika Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali pamoja na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka.

Naye Jaji Mkuu wa Tanzania, Mhe. Prof. Ibrahim Hamis Juma aliwataka wananchi pamoja na wadau wenye migogoro kutumia zaidi njia ya usuluhishi badala ya kukimbilia Mahakamani kwa kuwa tayari Ibara ya 107(2)(d) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1797 imetoa fursa kwa wadaawa kufanya usuluhishi, na hivyo usuluhishi utawasaidia wadaawa kupata haki pasipo kucheleweshwa bila sababu za msingi na pia kupata haki zao bila kutumia kanuni za kiufundi ambazo zimesababisha haki yingi kupotea bila sababu za msingi.

Mhe. Jaji Mkuu, alieleza kuwa faida nyingine za usuluhishi ni pamoja na kusaidia utatuzi wa migogoro kwa njia ya haraka, ufanisi na hivyo kuboresha mahusiano ya wadaawa; halikadhalika migogoro kwa njia hiyo unatunza faragha/usiri wa wadaawa; njia hiyo inaruhusu kupata ufafanuzi wa wataalam na pia njia ya kufanya usuluhishi zinaweza kubadilika.

Naye Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi alimuahidi Mhe. Rais Dkt. Samia kuwa Ofisi yake na ile ya



*Mawakili wa Serikali wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakiwa wamejipanga kwa ajili ya kushiriki Maadhimisho ya Kilele cha Wiki ya Sheria yaliyofanyika katika Viwanja vya Chinangali Jijini Dodoma.*

Wakili Mkuu wa Serikali wataendelea kusimamia vyema mashauri yote kwa niaba ya Serikali ikiwa ni pamoja na kutatua migogoro kwa njia ya usuluhishi pamoja na kusimamia kwa karibu maelekezo aliyoyatoa kuhusu jambo hilo ili kuhakikisha migogoro inatatuliwa kwa njia ya usuluhishi.

Hotuba hiyo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pia ilisomwa na Mawakili wa Serikali kwenye kilele cha maadhimisho hayo kwenye Mikoa yote ambayo ina Ofisi za Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

Maadhimisho hayo yalihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa Mahakama akiwemo Jaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania, Mhe. Prof. Ibrahim Hamis Juma, ambaye ndiye aliyekuwa mwenyeji wa Maadhimisho hayo, Majaji wa Mahakama ya Rufani, Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Mhe. Mustapher Siyani, Majaji wa Mahakama Kuu, Mtendaji Mkuu wa Mahakama, Prof. Elisante Ole Gabriel, Msajili Mkuu wa Mahakama, Mhe. Wilbert Chuma pamoja na watumishi wengine.

Wageni wengine walikuwa Jaji Mkuu wa Zanzibar, Mhe. Khamis Ramadhan Abdalla, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Tulia Ackson, Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro, Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama, Wakuu wa Wilaya, Viongozi wastaafu wa Mahakama na Serikali, Rais wa Chama cha Mawakili Tanganyika, Prof. Edward Hosea na wananchi kwa ujumla.



*Jaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania, Mhe. Prof. Ibrahim Hamis Juma akizungumza na viongozi na watumishi pamoja na wananchi (hawapo pichani) walioshiriki sherehe za kilele cha Siku ya Sheria nchini tarehe 01 Februari, 2023 katika Viwanja vya Chinangali jijini Dodoma.*




*Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi akisoma hotuba yake katika Sherehe za Maadhimisho ya kilele cha Siku ya Sheria nchini yaliyofanyika Jijini Dodoma.*



*Majaji wa Mahakama ya Rufani na Mahakama Kuu ya Tanzania wakisikiliza hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan tarehe 01 Februari, 2023 katika kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Sheria nchini yaliyofanyika katika Viwanja vya Chinangali jijini Dodoma.*



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Duncan Mwaipopo (aliyesimama katikati) akiwa kwenye picha ya pamoja na Mawakili wa Serikali wa Ofisi yake kwenye maadhimisho ya Kilele cha Wiki ya Sheria yaliyofanyika leo Jijini Dodoma.*

# Wadau Watakiwa Kutatua Migogoro kwa Njia ya Usuluhishi




**Mhe. Dkt. Philip Mpango**

**Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

**2023**

**Uzinduzi wa Wiki ya Sheria**

*Makamu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Mpango akizungumza na Wadau wa Mahakama (hawapo pichani) wakati wa uzinduzi wa Wiki ya Sheria uliofanyika katika viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma.*

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Mpango alisema kuwa utatuzi wa migogoro kwa njia usuluhishi unajenga maelewano na mapatano na kupelekea watu kuendelea kushirikiana baada ya mashauri kuisha.

Mhe. Dkt. Mpango alisema hayo akiongea na wadau wa sheria wakati wa uzinduzi wa Wiki ya Sheria uliofanyika katika Viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma na kusema kuwa “usuluhishi ni njia inayoweza kutumika pia kupunguza mlundikano wa kesi Mahakamani na kuepuka gharama kubwa za uendeshaji wa mashauri ambayo baadhi yake huchukua muda mrefu kukamilika”, alisema Dkt. Mpango.

Alisema kuwa utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi unaepusha visasi na hata wakati mwingine kuepusha watu kujichukulia sheria

mkononi na kuwahimiza wadau wa Mahakama na Sheria kuendelea na kampeni ya kutoa msaada wa kisheria kuhusu njia mbadala ya kutatua migogoro kwa njia ya usulushi.

“Mimi naamini migogoro mingi na hasa ile ya ardhi, mipaka na ile ya mirathi inaweza kutatuliwa kwa njia ya usuluhishi na kurejesha thamani kwa wananchi wetu”. alisema Mhe. Dkt. Mpango.

Dkt. Mpango amewataka wadau kuendelea kuchukulia kwa umuhimu na kulipa kipaumbele suala la utatuzi wa migogoro kwa njia usuluhishi ili kuenda sawa na kasi ya Mahakama katika kupunguza mashauri yaliyopo mahakamani.

Akimkaribisha Mgeni Rasmi, Jaji Mkuu wa Tanzania Mhe. Prof. Ibrahimu Hamis Juma alisema wananchi wengi wanajua kuwa nchi yetu inaongozwa na katiba, sheria na kanuni mbalimbali za utatuzi wa migogoro.

“Pamoja na uwepo wa Katiba na kanuni wananchi wengi hawafahamu namna ya kutumia kanuni na taratibu ili kutatua migogoro yao, wengi hawafahamu utatuzi wa migogoro kwa haraka una faida kwao binafsi na vile vile kwa uchumi wa nchi”, alisema Prof. Juma

Alisema Mahakama inafahamu wananchi wote wanaotafuta huduma mahakamani wanafahamu vyema haki na wajibu wao na taratibu za kimahakama na hiyo ndiyo sababu tumetenga wiki moja iwe ni wiki ya kukumbushana juu ya haki na jinsi ya kuzipata na kufahamu taasisi zilizopo kwenye mnyororo wa utoaji haki.

Prof. Juma alisema kuwa kauli mbiu ya Wiki ya Sheria ni umuhimu kwa utatuzi wa migogoro kwa njia usuluhishi katika kukuza uchumi endelevu ambapo inahimiza utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi ili kupunguza gharama za uendeshaji wa mashauri.

“usuluhishi unawezekana kama Mahakama, wadau na wananchi wataona faida ya usuluhishi kwa kuwa unatumia muda mfupi na gharama nafuu na kusaidia kukuza uchumi binafsi wa nchi kwa sababu unatumia muda mchache kutatua migogoro”, alisema Prof. Juma.

Katika wiki hiyo Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilishiriki kwa kuongozwa na Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo kwenye matembezi maalum yaliyoandaliwa na Mahakama ya Tanzania ikiwa ni pamoja na kutoa elimu ya msaada wa kisheria kwa wananchi na masuala mbalimbali yanayohusu Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na utekelezaji wa majukumu yake kwa wadau na wananchi kwa ujumla. Elimu hiyo kwa umma ilitolewa kwa njia mbalimbali ikiwemo kutembelea masoko, shule, magereza na kwenye vyombo vya habari pamoja na ugawaji wa vipeperushi, majarida kwa wadau waliotembelea banda la Ofisi. Kupitia maonyesho ya kwenye mabanda ufafanuzi ulitolewa kwenye maeneo kama sheria za ardhi, kazi, mikataba na usuluhishi.




*Jaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania, Mhe. Prof. Ibrahimu Hamis Juma akihutubia wakati wa uzinduzi wa Wiki ya Sheria kwenye Viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma.*




*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Mpango akiwa kwenye picha ya pamoja na wadau wa Mahakama wakati wa uzinduzi wa Wiki ya Sheria uliofanyika katika viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma.*



*Baadhi ya Majaji na wadau wa Mahakama wakimsikiliza Mgeni Rasmi Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Mpango (hayupo pichani) wakati wa uzinduzi wa Wiki ya Sheria uliofanyika kwenye viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma.*



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Mpango akiwa na Jaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania, Mhe. Prof. Ibrahim Juma, Jaji Mkuu wa Serikaki ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mhe. Khamis Ramadhan Abdallah, viongozi, watumishi na wananchi wa Mkoa wa Dodoma wakati akiongoza Matembezi ya Uzinduzi wa Wiki ya Sheria jijini Dodoma.*



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo (mwenye koti la bluu) akiwa kwenye matembezi maalum yaliyoandaliwa na Mahakama ya Tanzania kuashiria uzinduzi wa Wiki ya Sheria inayoambatana na utoaji wa msaada wa kisheria kwa wananchi jijini Dodoma.*




*Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro (Mb), akipata maelezo kuhusu majukumu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kutoka kwa Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Udhibiti Ubora alipotembelea banda la maonesho ya Ofisi hiyo kwenye Wiki ya Sheria iliyofanyika jijini Dodoma.*




*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo akipata maelezo kuhusu majukumu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kutoka kwa Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Udhibiti Ubora alipotembelea banda la maonesho ya Ofisi hiyo kwenye Wiki ya Sheria iliyofanyika jijini Dodoma.*



*Wakili Mfawidhi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wa Mkoa wa Dodoma, Bi. Jenipher Kaaya akijenga uelewa kuhusu majukumu ya Ofisi hiyo na msaada wa kisheria kwa baadhi ya wadau na wananchi wakati wa  Wiki ya Sheria iliyofanyika jijini Dodoma.*




*Baadhi ya watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakiwa kwenye picha ya pamoja ndani ya banda la maonesho ya Ofisi hiyo kwa ajili ya kutoa elimu ya msaada wa kisheria na majukumu ya Ofisi hiyo kwa wadau na wananchi wakati wa Wiki ya Sheria iliyofanyika jijini Dodoma.*



*Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Pauline Gekul (Mb), (aliyeketi katikati) akiwa kwenye picha ya pamoja na wajumbe wa Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali baada ya kikao na wajumbe hao kilichofanyika jijini Dar es Salaam alipofanya ziara kwa lengo la kujitambulisha na kujionea namna Ofisi hiyo inavyotekeleza makujumu yake, kushoto kwake ni Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende na kulia kwake ni Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo.*

# Naibu Waziri Gekul Aipongeza Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (OWMS) imepongezwa kwa kuendelea kuiwakilisha vyema Serikali katika kusimamia mashauri yaliyofunguliwa dhidi yake katika mahakama na mabaraza ya usuluhishi ndani na nje ya nchi.

Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Pauline Gekul (Mb) ametoa pongezi hizo alipotembelea Makao Makuu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali jijini Dar es Salaam kwa lengo la kujitambulisha na kufahamu namna Ofisi hiyo inavyotekeleza majukumu yake.

| Hadi Februari 2023 | |
|---|---|
| Jumla ya mashauri | |
| 6,263 | |
| madai | usuluhishi |
| 6,112 | 151 |

Mhe. Gekul ameipongeza OWMS kwa kuendelea kufanya kazi kwa bidii na kujitolea kwa kuiwakilisha Serikali kwenye mashauri mbalimbali pamoja na kuwa na rasilimali fedha chache na kuwataka kuendelea kuwa wazalendo.

Alisema kuwa Wizara ya Katiba na Sheria ni Wizara muhimu inayogusa wananchi wetu ambao wana haki zao nyingi ambazo wamekuwa wakizitafuta katika maeneo mbalimbali.

"Nafanya ziara kwenye taasisi zote zilizo chini ya Wizara hii ili nione mwelekeo kwa lengo la kuhakikisha tunafanya kazi kwa kushirikiana na kuwa wawazi ili tumsaidie na kumwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwenye nafasi hizi tulizo nazo," alisema Gekul.

Ameongeza kuwa Mhe. Rais Dkt. Samia amekuwa akifahamu mahitaji ya wananchi na amekuwa akigusa changamoto zao moja kwa moja kwa kuendeleza miradi mikubwa ya maendeleo, masuala ya afya na elimu ambayo kwa namna moja Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imekuwa ikihusika nayo.

Akisoma taarifa ya Ofisi Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende, Wakili Mkuu wa Serikali alisema kuwa jukumu kubwa la OWMS ni kuratibu, kusimamia na kuendesha mashauri yanayofunguliwa na Serikali na taasisi zake au dhidi ya Serikali na taasisi zake kwenye mahakama na mabaraza ya utoaji haki ndani na nje ya nchi.

Dkt. Luhende alisema kuwa OWMS imeendelea kuiwakilisha Serikali na taasisi zake kwa ufanisi katika mashauri yote ya madai na usuluhishi ambapo hadi kufikia mwezi Februari, 2023; OWMS imesajili jumla ya mashauri 6,263 ambapo kati ya hayo mashauri ya madai ni 6,112 na mashauri ya usuluhishi 151 na hivyo kazi hii ya OWMS imeiwezesha Serikali kuepuka gharama kubwa za Mawakili wa kujitegemea.

"Tumeendelea kusimamia mashauri hata kwenye taasisi binafsi ambazo Serikali ina maslahi mfano Kampuni ya Simu ya Airtel Tanzania na baadhi ya benki," alisema Dkt. Luhende.

Dkt. Luhende aliongeza kuwa OWMS imefanikiwa kuongoza na kushiriki katika Timu za Serikali za Majadiliano na kufanikisha kumaliza mashauri na migogoro mbali mbali kwa njia ya majadiliano, usuluhishi na maridhiano nje ya Mahakama.

Aidha, Dkt. Luhende alisema maeneo ya vipaumbele vya OWMS ni kuendelea kuwajengea uwezo watumishi kwa kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi ikiwemo mafunzo ya ubobevu katika maeneo mtambuka kama vile ya nishati, gesi na uwekezaji.

Alisema OWMS inaendelea kuimarisha mifumo ya kidijitali ikiwa ni sehemu ya kuboresha mfumo wa usimamizi wa mashauri ili kuhakikisha mifumo ya OWMS inasomana na mifumo ya taasisi nyingine tunazoshirikiana nazo.

Naye Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo akifafanua kuhusu fedha za miradi ya maendeleo alieleza kuwa katika Mwaka wa Fedha 2023/24, OWMS kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka zina mpango wa pamoja wa kujenga vituo jumuishi kwenye mikoa mbali mbali kwa lengo la kusogeza huduma kwa wananchi na kupunguza gharama za pango la Ofisi. Kupitia mpango huo, OWMS inatarajia kujenga Ofisi hizo kwenye mji wa Dodoma na Tabora na tayari imeandaa andiko kwa ajili ya kujenga hoja ya kupata fedha za mradi wa maendeleo za ujenzi wa majengo ya vituo jumuishi.



# Taarifa ya Utekelezaji ya Nusu Mwaka wa Fedha 2022/23

*Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Pauline Gekul (Mb), (aliyesimama kulia) akipokea taarifa ya utekelezaji ya nusu Mwaka wa Fedha 2022/23 ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kutoka kwa Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende baada ya ziara kwenye Ofisi hiyo jijini Dar es Salaam. Aliyesimama katikati akishuhudia ni Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Bi. Sarah Mwaipopo.*



*Mhe. Pauline Gekul (Mb), akiwasalimia watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali mara baada ya kuwasili kwenye Ofisi hiyo jijini Dar es Salaam kwa lengo la kujitambulisha na kujionea namna inavyotekeleza majukumu yake.*




*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende (wa pili kushoto) akimuonesha vitabu vya mashauri ya usuluhishi Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Pauline Gekul (Mb), (wa pili kulia) alipotembelea Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali jijini Dar es Salaam kwa lengo la kujitambulisha. Wa kwanza kulia ni Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo na wa kwanza kushoto ni Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Utafiti na Huduma za Maktaba, Kiuye Shemakame.*



*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende (wa kwanza kulia) akimuonesha Mhe. Pauline Gekul (Mb), Naibu Waziri wa Katiba na Sheria mazingira ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakati wa ziara ya Naibu Waziri huyo alipotembelea Ofisi hiyo kwa mara ya kwanza tangu ateuliwe kushika nafasi hiyo. Anayefuata ni Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo.*



*Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Pauline Gekul (aliyesimama katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende (wa kwanza kulia) na Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo (aliyesimama kushoto) baada ya kikao chake na Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kilichofanyika jijini Dar es Salaam.*



*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende (aliyesimama katikati) akiwa kwenye picha ya pamoja na Kaimu Mtendaji Mkuu wa TLS, Bi. Mariam Othman (wa pili kutoka kulia) na Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo (wa pili kutoka kushoto) pamoja na viongozi wengine wa Ofisi hizo mara baada ya kikao kilichofanyika kwenye Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali jijini Dar es Salaam.*

# TLS Yatakiwa Kuwajengea Uwezo Wanachama Wake

Wakili Mkuu wa Serikali amekitaka Chama cha Mawakili wa Tanganyika (TLS) kuendelea kuwajengea uwezo wanachama wake ili waweze kufanya kazi kwa pamoja kwenye maeneo ambayo yanauhitaji mkubwa wa wabobezi wa maeneo mahususi.

Hayo yameelezwa na Dkt. Boniphace Luhende, Wakili Mkuu wa Serikali akiwa Ofisini kwake alipokutana na Kaimu Mtendaji Mkuu wa Chama cha Mawakili Tanganyika, Bi. Mariam Othman aliyefika Ofisini kwake kwa ajili ya kujitambulisha. Utambulisho huo ulihudhuriwa na kushuhudiwa na baadhi ya viongozi wa Ofisi hiyo akiwemo Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo.

Alisema kuwa changamoto iliyopo kwa sasa ni kuwa ni ukosefu wa Mawakili ambao wamejikita katika eneo moja la ubobezi na kufanya kazi kwa malengo hivyo ni vyema Mawakili wakatengenezwa ili waweze kufanya kazi na kuzitangaza kazi zao ili waweze kutumika kwenye kazi za Serikali.

Dkt. Luhende alisema kuwa anafahamu namna TLS inavyoshirikiana na taasisi za Serikali na kuipongeza Menejimenti ya TLS kwa kufanya kazi vizuri na kwa kutambua kuwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ni wadau wa TLS.

"Mdau mkubwa wa TLS ni Serikali kwa sababu ndio muajiri mkubwa na wanachama wengi wa TLS wanatoka hapo na ndio ina watu wengi na miradi mikubwa hivyo huwezi kuikwepa Serikali," alisisitiza Dkt. Luhende.

Aliwataka TLS kufanya utafiti kwenye mada wanazozitoa kwenye semina mbali mbali ili ziendane na mahitaji ya wanachama wao ili waajiri waone umuhimu wa kuwapeleka Mawakili kuhudhuria semina hizo.

Dkt. Luhende alisema kuwa TLS wana jukumu la kuhakikisha kwamba Mawakili wanakaa kwenye mstari kwa kuendelea kuwakumbusha Mawakili misingi ya taaluma zao na maadili ili kuitendea haki Sekta ya Sheria nchini na wadau wanaowahudumia.

Naye Kaimu Mtendaji Mkuu wa TLS Bi. Mariam Othman ambaye aliambatana na ndugu Kaleb Gamaya, Mtendaji Mkuu wa TLS aliyemaliza muda wake, aliiomba Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kuendeleza ushirikiano uliopo kwa kuwafanya Mawakili wa Serikali kuwa wanachama hai na kuendelea kushiriki katika chama hicho.

"Tumeona ni vyema kufika kuonana na wewe ili tujitambulishe na kuomba ushirikiano huo kwa kuwa Mawakili wengi wa Serikali pia ni wanachama wa TLS," alisema Bi. Othman.

Pia, Bi. Othman ameomba Mawakili wa TLS ambao sio waajiriwa wa Serikali kupewa nafasi na kushiriki kuendesha mashauri ya usuluhishi ili zinapotokea kazi ambazo wanaweza kufanya chama hicho kitoe Mawakili hao wenye uzoefu.

Naye Mkurugenzi Msaidizi Udhibiti Ubora wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Mercy Kyamba aliishukuru TLS kwa kuendelea kufanya kazi kwa vitendo na kudumisha ushirikiano na Ofisi hizi mbili na kuwaomba kuangalia jinsi ya kuwafutia Mawakili wa Serikali ambao ni wanachama wa TLS malimbikizo ya ada za uanachama.

Pia, Mkurugenzi Msaidizi wa Mashauri ya Madai ya Ndani wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Deodatus Nyoni alisema kuwa TLS iweke utaratibu wa kuwapatia cheti cha uzoefu cha uendeshaji wa mashauri Mawakili wa Serikali wanaohudhuria mafunzo kwa vitendo kwa kushiriki uendeshaji wa mashauri kwenye Mahakama za Rufaa na mikutano mbali mbali ya Mawakili kwa kuwa wanapata uzoefu na kuongeza ujuzi katika taaluma yao.



*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende akizungumza na Kaimu Mtendaji Mkuu wa TLS, Bi. Mariam Othman pamoja na ujumbe wake (hawapo pichani) kuhusu masuala mbalimbali yenye lengo la kuongeza ushirikiano kati ya Ofisi hizo mbili kwenye kikao kilichofanyika kwenye Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, jijini Dar es Salaam.*



*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende (aliyesimama kushoto) akimkabidhi Jarida la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Kaimu Mtendaji Mkuu wa Chama cha Mawakili wa Tanganyika (TLS), Bi. Mariam Othman ambaye alimtembelea kiongozi huyo kwa lengo la kujitambulisha tarehe 07/03/2023 Ofisini kwake jijini Dar es Salaam.*



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo (aliyesimama kushoto) akimkabidhi Kaimu Mtendaji Mkuu wa Chama cha Mawakili wa Tanganyika (TLS), Bi. Mariam Othman Kalenda ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali mara baada ya kumalizika kikao baina ya viongozi hao. Kikao hicho kilifanyika katika Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali iliyopo Jijiji Dar es Salaam.*

# Serikali Yasisitiza Uzingatiaji wa Usawa wa Kijinsia, Ubunifu na Mabadiliko ya Teknolojia



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo (aliyesimama katikati) akiwa katika picha ya pamoja na wanawake wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali mara baada ya kumaliza kikao kwa ajili ya kujadili kauli mbiu ya Siku ya Wanawake Duniani kwenye ukumbi wa mikutano wa Ofisi hiyo jijini Dar es Salaam.*

Serikali imepiga hatua kubwa katika kuhakikisha kwamba masuala ya usawa wa kijinsia kwa ujumla yanapewa kipaumbele na wanawake wanashirikishwa kwenye masuala ya kidijitali, uvumbuzi na teknolojia nchini.

Kauli hiyo ilitolewa na Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo alipokuwa akiongea

na wanawake wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yenye kauli mbiu "Ubunifu na Mabadiliko ya Teknolojia ni Chachu katika kuleta Usawa wa Kijinsia".

Alisema kauli mbiu ya mwaka huu inawataka wanawake kuhakikisha kwamba katika safari ya kuelekea kwenye usawa wa kijinsia katika ngazi zote wanakuwa ni wabunifu na wenye uwezo na maarifa ya kuendana na kasi ya mabadiliko ya kiteknolojia. Aidha, wanawezeshwa kutumia mifumo na nyenzo mbalimbali za kidijitali na kupatiwa mafunzo ya masuala ya kiteknolojia.

"Kauli mbiu hii inatuhamasisha sisi wanawake katika kuhakikisha kwamba tunaitumia siku hii kama fursa ya kushiriki kikamilifu kuainisha mafanikio, changamoto na mahitaji yetu yanayohusiana na masuala ya kidijitali na kiteknolojia na kushauriana namna bora ya kuandaa mikakati ya utekelezaji," alisema Mwaipopo.

Alisema kuwa Ibara ya 13 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,1977 inasisitiza masuala ya usawa wa kijinsia kwenye nyanja zote sambamba na sheria mbalimbali, kanuni na sera ambazo Serikali inasimamia na kufanikisha utekelezaji wake.

"Serikali imesaini mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa ambayo nayo inasisitiza masuala ya kijinsia katika maeneo yote ikijumuisha masuala ya uvumbuzi na teknolojia. Sote tunafahamu ya kwamba tupo katika karne ya 21 ambayo kila kitu kinafanyika kwa kutumia teknolojia na nyenzo



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Bi. Sarah Mwaipopo (mwenye kitenge begani) akiwa katika picha ya pamoja na wanawake wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kabla ya kuelekea kwenye viwanja vya mnazi mmoja kushiriki kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani. Aliyeshika vuvuzela ni Mwenyekiti wa Wanawake TUGHE Tawi la Ofisi hiyo, Bi. Celina Togocho.*



*Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Mhe. Amos Makala ambaye alikuwa Mgeni Rasmi akizungumza na watumishi wa Serikali, taasisi binafsi, asasi za kiraia pamoja na wananchi walioshiriki Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani iliyofanyika kimkoa katika Viwanja vya Mnazi Mmoja vilivyopo jijini Dar es Salaam.*

za kidijitali kwa hiyo hakuna nchi inayoweza kuendelea au kupata maendeleo bila ya kuwa na teknolojia", alisema Mwaipopo.

Aliwataka wanawake katika Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kuhakikisha wanashiriki na kushirikishwa kwenye masuala ya kiteknolojia kwa kupatiwa fursa kwa kadri bajeti na rasilimali fedha inavyoruhusu ili kuwawezesha kutekeleza vyema majukumu ya usimamizi na uendeshaji mashauri ya madai na usuluhishi katika ngazi zote ambazo mashauri husika yanapokelewa, kusajiliwa, kuandaliwa nyaraka na kupatiwa uwakilishi Mahakamani.

Katika hatua nyingine, Watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, walishiriki maadhimisho ya siku ya wanawake duniani kwenye Viwanja vya Mnazi Mmoja Dar es salaam. Naye Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Mhe. Amos Makala ambaye alikuwa Mgeni Rasmi wa kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani kwa Mkoa wa Dar es Salaam alisema kuwa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alisema katika mkoa wake ameendelea kuwawezesha wanawake mkoani humo ili kuhakikisha wanasimama vyema katika nyanja zote ikiwemo masuala ya kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Alisema kuwa kufikia mwezi Machi mwaka huu, Serikali mkoani Dar es Salaam imefanikiwa kutoa mikopo nafuu kwa wanawake wanaofanya shughuli

mbalimbali mkoani humo ambapo katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2022/2023 kiasi cha shilingi bilioni 13.9 zilitengwa na kutolewa kwa wanawake ikiwemo vijana na wenye ulemavu.

Makala ametoa wito kwa wananchi wa mkoa wa Dar es Salaam kujiunga kwenye vikundi na kuvisajili ili waweze kunufaika na fursa mbalimbali zilizopo katika halmashauri zote za Jiji la Dar es Salaam.

“Natoa wito kwa wananchi wa mkoa wa Dar es Salaam kujiunga kwenye vikundi vilivyosajiliwa ili waweze kunufaika na fedha mbalimbali ndani ya halmashauri zote za Jiji la Dar es Salaam,” alisema Mhe. Makala.

Kuhusu umuhimu wa maadhimisho haya Mhe. Makala ameeleza kuwa maadhimisho haya yanajenga hamasa na ushiriki katika kuchangia na kuleta usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake katika kutekeleza masuala mbalimbali ikiwemo kuimarisha mifumo ya kijamii na hamasa kwa jamii kwa minajili ya kuleta usawa wa kijinsia, kuongeza msukumo wa ushiriki wa wanawake katika uongozi na vyombo vya kutoa maamuzi, kubadilishana taarifa na uzoefu kuhusu masuala ya jinsia na uwezeshaji wanawake, utekelezaji wa maazimio, mikataba na itifaki za kimataifa ambazo nchi yetu imeridhia.

Faida nyingine za maadhimisho haya ni kushirikisha na kutoa mrejesho kwa wananchi kuhusu hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa mikataba ya kimataifa na kikanda pamoja na mipango ya sera za kitaifa, kisekta kuhusu masuala ya usawa wa kijinsia na uwezeshaji wananchi kiuchumi na kijamii.

Alifafanua kuwa nchi yetu pia inatambua umuhimu na mchango wa mwanamke katika siasa, jamii na uchumi hivyo mwaka huu nchi yetu inaungana na nchi nyingine duniani kuadhimisha Siku ya Wanawake kama ambavyo na sisi mkoa wa Dar es Salaam tunaadhimisha siku hii muhimu.



*Baadhi ya wanawake kutoka Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakisherehekea kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yaliyofanyika katika Viwanja vya Mnazi Mmoja Jijini Dar Es Salaam.*

Akizungumzia kauli mbiu ya mwaka huu inayosema, “Ubunifu na Mabadiliko ya Teknolojia: Chachu katika kuleta Usawa wa Kijinsia”, Mhe. Makala alisema kuwa kauli mbiu hii inaenda kuelimisha, kuhimiza, na kuhamasisha umma kuhusu umuhimu wa uwepo wa haki na usawa katika jamii katika kufikia malengo endelevu hivyo wadau mbalimbali wa maendeleo ya wanawake nchini, viongozi wa Serikali, siasa, dini, na asasi za kiraia tuungane wote kwa pamoja katika kutekeleza kauli mbiu hii.

Ifahamike kuwa Siku ya Kitaifa ya Wanawake Duniani ilianza mwaka 1911 kufuatia maandamano ya wanawake wafanyakazi wa viwandani nchini Marekani waliokuwa wakipinga mazingira duni ya kazi kama vile ukosefu wa huduma za kijamii na unyanyasaji katika ajira, hivyo kuendelea kuadhimisha Siku hiyi ni kuenzi mchango wa wanawake katika ujenzi wa Taifa.

Kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani katika mkoa wa Dar es Salaam kilifanyika katika Uwanja wa Mnazi Mmoja yakitanguliwa na maandamano ya wanawake kutoka taasisi mbalimbali za Serikali, ikiwemo Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, mashirika binafsi na asasi za kiraia yaliyoanzia katika Viwanja vya Mashujaa vilivyopo eneo la Mnazi Mmoja Dar es Salaam.



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo (aliye katikati) akiongoza maandamano ya wanawake kutoka Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Dar es Salaam kuelekea Uwanja wa Mashujaa kwa ajili ya kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani mkoa wa Dar es Salaam. Kushoto kwake ni Mwenyekiti wa Wanawake TUGHE Tawi la Ofisi hiyo, Bi. Celina Togocho.*



*Mkaguzi Mkuu wa Ndani Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Joan John akizungumza na washiriki wa mafunzo elekezi ya utunzaji wa nyaraka za Serikali (hawapo pichani) wakati akifungua mafunzo ya siku tatu kwa watumishi hao yaliyofanyika mkoani Morogoro.*

# Zingatieni Uadilifu na Usiri wa Nyaraka za Serikali

Makatibu Sheria watakiwa kuzingatia uadilifu, usiri, kanuni, taratibu na sheria mbalimbali zinazosimamia utunzaji wa nyaraka za Serikali katika utendaji wao wa kazi na kuepuka kuwa chanzo cha kuvujisha nyaraka hizo kinyume na taratibu.

Hayo yamesemwa na Mkaguzi Mkuu wa Ndani Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Joan John alipokuwa anafungua mafunzo elekezi ya utunzaji wa nyaraka za Serikali kwa niaba ya Naibu Wakili Mkuu wa Serikali kwa Makatibu Sheria kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali yaliyofanyika mkoani Morogoro.

Bi. Joan aliwataka watumishi hao kuwa makini na kutumia ujuzi wa mafunzo

wanayoyapata kuondoa hali ya uvujaji wa nyaraka za Serikali katika mitandao ya kijamii kwa maslahi yao binafsi na kupelekea kujadiliwa katika mitandao hiyo kinyume cha utaratibu.

"Sitarajii kuona mshiriki wa mafunzo haya anakuja kuwa na tuhuma za uvujishaji wa nyaraka kwani natumai kuwa tutakuwa tumejua madhara ya kufanya hivyo na Serikali haitakuwa na muamana na mtumishi atakayebainika kuhusika na uvujishaji wa taarifa zake za aina yoyote," Alisema Bi. Joan

Alisema kuwa Masijala ya Sheria ni eneo nyeti katika Ofisi ambapo ndipo nyaraka za mashauri zinapopokelewa, kuhifadhiwa na kusambazwa hivyo ni muhimu Makatibu wa Sheria kuzingatia utunzaji wa siri wa nyaraka hizo.

Aliwataka washiriki wa mafunzo hayo muhimu kujitathmini utendaji wao wa kazi na kupata fursa ya kukumbushwa miiko na taratibu za kiutendaji hasa katika usiri na utunzaji wa nyaraka za Serikali kwa njia ya kieletroniki.

Bi. Joan aliwataka pia washiriki kuwa wasikivu na huru kutoa maoni, mapendekezo na kushirikisha ujuzi wao katika mambo ya kiofisi ili kusaidia kuleta uelewa mpana na hatimaye ufanisi pindi wanapomaliza mafunzo yao.



*Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Masijala ya Sheria wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Dennice Leonard akimkaribisha Mgeni Rasmi (hayupo pichani) Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Ofisi hiyo, Bi. Joan John kufungua mafunzo ya siku tatu kuhusu utunzaji wa nyaraka za Serikali yaliyofanyika mkoani Morogoro.*

Akimkaribisha mgeni rasmi, Mkuu wa Kitengo cha Masijala ya Sheria, ndugu Dennice Leonard alisema kuwa mafunzo hayo elekezi yamejumuisha watumishi 25

kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

Leonard alisema kuwa lengo la mafunzo hayo ni kuwawezesha watumishi kubadilishana uzoefu kwenye masuala ya utunzaji wa kumbukumbu za kieletroniki na kuendeleza mashirikiano baina ya Ofisi hizo tatu.

"Matarajio yetu baada ya mafunzo haya ni kuhakikisha tunakuwa na utunzaji sahihi wa kumbukumbu za kieletroniki ambao utaleta matokeo chanya katika Ofisi zetu na pia yatatusaidia kufahamu aina ya nyaraka zinazoruhusiwa na zisizoruhusiwa kusambazwa kwa njia ya kieletroniki", alisema Leonard.

Naye mshiriki wa mafunzo hayo Katibu Sheria, ndugu Ally Ally alisema kuwa mafunzo hayo yatawawezesha kutekeleza majukumu yao kwa vitendo ili kuongeza ufanisi wa kazi katika maeneo yao ya utunzaji wa nyaraka za Serikali.

"Matarajio baada ya mafunzo haya ni kuongeza ufanisi kwenye utendaji kazi wetu na kuhakikisha Kitengo chetu hakitakuwa chanzo cha kuvujisha taarifa na kuzisambaza katika mitandao ya kijamii bali tutaenda kusimamia kanuni, taratibu na sheria za nchi," alisema Ally.



*Baadhi ya Washiriki wa mafunzo ya Utunzaji wa nyaraka za Serikali kutoka Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka wakimsikiliza Mgeni Rasmi, Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Joan John (hayupo pichani) wakati wa ufunguzi wa mafunzo hayo mkoani Morogoro.*



*Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Bi Joan John (kushoto) akiteta jambo na Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Masijala ya Sheria wa Ofisi hiyo, Dennice Leonard kabla ya kufungua mafunzo elekezi ya utunzaji wa nyaraka za Serikali yaliyofanyika mkoani Morogoro.*



*Katibu Sheria wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, ndugu Ally Ally akimsikiliza kwa makini mtoa mada ya maadili ya usalama na utunzaji wa nyaraka za Serikali (hayupo pichani) katika mafunzo yaliyofanyika mkoani Morogoro.*

JAMHURI WA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI

OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI
10 Barabara ya Kivukoni
S. L. P 71554
11101 DAR ES SALAAM

Simu: +255 22 2127384
Fax: +255 22 2127385
Nukushi: www.osg.go.tz
Barua pepe: info@osg.go.tz

## ANUANI ZA POSTA NA MAENEO ZILIPO OFISI ZA WAKILI MKUU WA SERIKALI MIKOANI

| | |
|---|---|
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 1902<br>41218 DODOMA<br>Jengo la Katiba na Sheria (UDOM)<br>Barua pepe: dodoma@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 130<br>31101 MUSOMA<br>Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: mara@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 1280<br>63114 MTWARA<br>Maadili House<br>Barua pepe: mtwara@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 394<br>33101 MWANZA<br>Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: mwanza@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 595<br>51108 IRINGA<br>Lilokuwa jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Iringa<br>Barua pepe: iringa@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 106<br>35102 BUKOBA<br>Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Mhakiki Mali<br>Barua pepe: kagera@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 564<br>57101 SONGEA<br>Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: ruvuma@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 43<br>37101 SHINYANGA<br>Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: shinyanga@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 60<br>21101 TANGA<br>Jengo la Mkonge<br>Barua pepe: tanga@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 119<br>45112 TABORA<br>Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: tabora@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 202<br>25101 MOSHI<br>Jengo la TRA Moshi<br>Barua pepe: kilimanjaro@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 690<br>55103 SUMBAWANGA, Mtaa wa Ukaguzi<br>Jengo la Ukaguzi, Gorofa ya pili<br>Barua pepe: rukwa@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 66<br>23101 ARUSHA<br>Jengo la AICC, Arusha<br>Barua pepe: arusha@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 710<br>53107 MBEYA<br>Jengo la Madini<br>Barua pepe: mbeya@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 172<br>47101 KIGOMA, Jengo la NHC, Ghorofa ya Pili,<br>Kiwanja Na. 148 & 149, Mtaa wa Lumumba.<br>Barua pepe: kigoma@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>Jengo la NSSF, Ghorofa la Nne<br>MOROGORO, Barabara ya zamani DSM<br>Barua pepe: morogoro@osg.go.tz |